

NENO LA KUMKARIBISHA MGENI RASMI NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI MHE.MWITA WAITARA (MB) KATIKA UZINDUZI WA TOVUTI YA BARAZA LA USHAURI LA WATUMIAJI WA HUDUMA ZA USAFIRI ARDHINI (LATRA CCC) TAREHE 01 OCTOBA 2021

**MH. Mwita Waitara, (MB) Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi,
Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya ya Temeke, Kigamboni, Ilala,
Kinondoni na Ubungo,**

**Wakuu wa taasisi mbalimbali za Serikali na sekta binafsi,
Wajumbe wa Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za
Usafiri Ardhini,**

**Wawakilishi wa Majukwaa ya Wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha
Dar es Salaam,**

**Wawakilishi wa Vilabu vya Wanafunzi wa Sekondari na Shule za
Msingi za Mkoa wa Dar Es Salaam;**

Wageni waalikwa,

Sekretariati ya Baraza,

Wanahabari,

Mabibi na mabwana.

Nawasalimu kwa Jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Awali ya yote ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa zawadi ya uhai na kwa kutujalia neema ya kukutana hapa kwa ajili ya uzinduzi wa tovuti ya Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Usafiri Ardhini. (LATRA CCC). Nakukaribisha sana katika Mkoa wetu wa Dar es Salaam. Wewe na Wageni wengine wote kutoka Nje ya Dar es Salaam. **Karibuni sana.**

Mh. Naibu Waziri,

Dar Es Salaam, ni Jiji lenye watu wengi zaidi ya miji yote Tanzania, Ni Jiji lenye shughuli nyingi za kiuchumi, zaidi ya miji yote Tanzania. Ni Jiji lenye Miundombinu mikubwa na Mizuri Zaidi ya miji yote Tanzania, tuna barabara za Juu, nyingine zinapita juu ya Bahari, ni furaha kubwa na Pongezi nyingi za dhati, kwa Mh. Rais Wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mh. Samia Suluhu Hassan, na kwa Mh. Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi na timu yake kwa kazi nzuri na kwa usimamizi mahiri. **Hongereni sana.**

Mh. Naibu Waziri,

Nimesikia, kwenye taarifa ya Baraza juu ya Changamoto mbalimbali zinazokabili watumiaji wa Huduma za Usafiri Ardhini. Zikitajwa kwa uwazi, dhahama wanazokumbana nazo wakazi wa Dar es Salaam. Ni kiri tu kwa kusema, Watumiaji wa Huduma za Usafiri Jijini Dar Es Salaam wanakumbana na changamoto nyingi, zipo changamoto ambazo, kwa kweli tunaweza kuziondoa, hata bila kuhitaji fedha. Mfano tabia ya Abiria kuingia kwenye vyombo vya Usafiri kwa fujo.

Hii ni tabia inayokera na haileti afya kwa watoto wetu wa shule za msingi, sekondari, walemavu, wajawazito, na wazee. Naunga mkono jitihada hizi za Baraza za kuelimisha umma juu ya Ustaarabu kwenye vyombo vya Usafiri.

Pili, suala la kutumia tiketi mtandao kwenye Usafiri wa umma. Mimi naona Tanzania tumechelewa sana. Faida za tiketi mtandao ni nyingi sana kwa Wamiliki wa vyombo, Abiria na Serikali kwa ujumla. Pengine, tungesisitiza matumizi ya teknolojia, yangesaidia

sana kuwa na Jiji lenye nguvu kubwa sana ya Kiuchumi katika Afrika Masharini na Afrika kwa Ujumla.

Tatu, Kuwepo kwa migogoro mingi kati ya abiria na watoa Huduma ni kukosekana kwa usimamizi madhubuti, kwa Wamiliki wa vyombo vya Usafiri. Ifike mahali sasa, katika Wilaya zetu zote, kwa kushirikiana na Taasisi ya Udhubiti na Usimamiaji wa Sheria, tuwe na kauli moja ya Wamiliki wa vyombo kuboresha Huduma zao, ili walaji wa Huduma hizi waweze kuona thamani ya fedha zao wanazolipa kama nauli.

Mh. Naibu Waziri,

Kama Mkoa, tunamambo mengi sana ya kuzungumza katika kuboresha Huduma za Usafiri Ardhini, ila kwa Siku ya leo, nimeombwa kukukaribisha wewe, ili uweze kuongea na Washiriki hawa kwenye huu uzinduzi wa tovuti ya Baraza la LATRA CCC.

Nikuombe sasa Mh. Naibu Waziri (Mb) karibu kuongea na hadhara hii.

KARIBU SANA.